



**MUHTASARI WA PATO LA TAIFA
ROBO YA NNE (OKTOBA – DESEMBA) 2025
BEI ZA MWAKA WA KIZIO 2015**



Machi, 2026



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**MUHTASARI WA PATO LA TAIFA
ROBO YA NNE (OKTOBA - DESEMBA) 2025
BEI ZA MWAKA WA KIZIO 2015**



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Wizara ya Fedha

Dodoma

Machi, 2026

Yaliyomo

Yaliyomo	i
Orodha ya Majedwali	iii
Orodha ya Vielelezo	iv
Orodha ya Viambatisho	v
Dibaji	vi
1.0. Utangulizi	1
1.1. Uchumi wa Dunia	1
1.2. Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara	1
1.3. Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika	1
1.4. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki	2
1.5. Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa Nchini Tanzania	3
1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Nne ya Mwaka 2025	3
1.5.2 Mchango wa Makundi Makuu ya Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa	4
1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi, Robo ya Nne ya Mwaka 2025	5
1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Nne ya Mwaka 2025	6
2.0. Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi	6
2.1. Kilimo, Misitu na Uvuvi	7
2.1.1. Mazao	7
2.1.2. Mifugo	8
2.1.3. Misitu	8
2.1.4. Uvuvi	8
2.2. Uchimbaji wa Madini na Mawe	8
2.3. Uzalishaji Viwandani	9
2.4. Umeme	9
2.5. Usambazaji Maji	10
2.6. Ujenzi	11
2.7. Biashara na Matengenezo	11
2.8. Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo	12

2.9. Malazi na Huduma ya Chakula	12
2.10. Habari na Mawasiliano	12
2.11. Fedha na Bima	13
2.12. Upangishaji Majengo	13
2.13. Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi.....	13
2.14. Huduma zinazohusiana na Utawala	14
2.15. Utawala na Ulinzi	14
2.16. Elimu	14
2.17. Afya na Huduma za Jamii	15
2.18. Sanaa na Burudani	15
2.19. Huduma Nyingine za Jamii	15
3.0. Hitimisho	16
Viambatanisho:	17

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Thamani ya Pato la Taifa (TZS Milioni), Robo ya Nne Mwaka 2021-2025	4
Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Baadhi ya Madini kwa Robo ya Nne ya Mwaka 2024 na 2025	9

Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Robo ya Nne ya Mwaka 2024 na 2025	2
Kielelezo Na 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Nne Mwaka 2021 – 2025.....	3
Kielelezo Na. 3: Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Nne ya Mwaka 2021 - 2025.....	4
Kielelezo Na. 4: Mchango wa Makundi Makuu ya Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Robo ya Nne 2025	5
Kielelezo Na.5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi, Robo ya Nne ya Mwaka 2025.....	6
Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Nne ya Mwaka 2024 na 2025.....	7
Kielelezo Na. 7: Uzalishaji wa Maji, Robo ya Nne Mwaka 2021 – 2025	11
Kielelezo Na. 8: Thamani ya Mikopo na Amana (TZS Trilioni), Robo ya Nne ya Mwaka 2021 – 2025	13

Orodha ya Viambatisho

Kiambatisho Na. 1:	Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 - Sh. Milioni.....	17
Kiambatisho Na. 2:	Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Asilimia	21
Kiambatisho Na. 3:	Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni	25
Kiambatisho Na 4:	Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Asilimia.....	29

Dibaji

Ukokotoaji wa Takwimu za Pato la Taifa unazingatia Mwongozo wa Umoja wa Mataifa wa Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa wa Mwaka 2008 (*System of National Accounts 2008*) na Mwongozo wa Kimataifa wa Kuainisha Shughuli zote za Kiuchumi (*International Standard Industrial Classification of All Economic Activities (ISIC), Rev. 4*). Ukokotoaji wa Pato la Taifa kwa kuzingatia miongozo hii huwezesha kupatikana kwa takwimu linganifu za robo mwaka kati ya Tanzania Bara na za mataifa mengine.

Matokeo katika ripoti za robo mwaka husaidia kufanya mapitio ya mara kwa mara ya sera na maendeleo ya kiuchumi ya muda mfupi. Vipindi vya “robo” vilivyotumika kuwakilisha Kalenda ya mwaka ni: Robo ya kwanza - Januari – Machi; Robo ya pili- Aprili – Juni; Robo ya tatu-Julai – Septemba na robo ya nne - Oktoba – Desemba. Vyanzo vya taarifa vinahusisha takwimu za utawala za shughuli zote za kiuchumi zilizofanyika katika kipindi cha rejea.

Ripoti ya Pato la Taifa kwa Robo ya nne ya Mwaka 2025 inabainisha jumla ya thamani ya bidhaa na huduma kwa aina ya shughuli za kiuchumi kwa bei za mwaka husika na bei za mwaka wa kizio wa 2015. Aidha, taarifa nyingine zilizowasilishwa katika ripoti hii ni mchango kwenye Pato la Taifa na kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi.

Ninatambua na kuthamini kwa dhati mchango wa wadau wa takwimu pamoja na Taasisi za Umma na Binafsi uliowezesha upatikanaji wa taarifa za msingi zilizotumika katika uchambuzi na uandaaji wa ripoti hii. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kushirikiana na wadau katika kuboresha mifumo ya kitakwimu na kupanua wigo wa upatikanaji wa takwimu za msingi kwa ajili ya kupima mwenendo wa shughuli za kiuchumi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.



Dkt. Amina S. Msengwa

Mtakwimu Mkuu wa Serikali

1.0. Utangulizi

Pato la Taifa kwa robo mwaka ni kiashiria chenye taarifa za kina za mwenendo wa ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika nchi. Kiashiria hiki hutumika kutathmini mwenendo wa ukuaji na mchango wa shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa katika vipindi vifupi kwa lengo la kutunga, kutathmini na kufuatilia sera za kiuchumi kwa wakati muafaka katika nchi.

1.1. Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) Kupitia *World Economic Outlook (WEO)* toleo la Januari 2026, ukuaji wa uchumi wa dunia utakuwa kwa kiwango cha asilimia 3.3 mwaka 2025 kutoka asilimia 3.2 kilichokadiriwa katika ripoti ya mwezi Oktoba 2025. Kuongezeka huku kunachangiwa na sababu mbalimbali. Kwanza athari za mvutano wa kibiashara zilikuwa ndogo kuliko ilivyotarajiwa awali, hali iliyosaidia kupunguza athari hasi kwenye biashara za kimataifa. Pili, kumeshuhudiwa ongezeko la uwekezaji katika teknolojia za kisasa, hususan akili unde na miundombinu ya kidijitali. Aidha, kuboreka kwa hali ya masoko ya fedha pamoja na sera za uchumi zilizoendelea kusaidia mahitaji ya jumla zimeimarisha matumizi na uwekezaji. Vile vile utendaji bora kuliko matarajio katika uchumi mkubwa hususan Marekani na China, umechangia kiasi kikubwa katika marekebisho ya ukuaji.

1.2. Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara


Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Fedha Duniani (IMF) WEO ya mwezi Januari 2026, ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara unakadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 4.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.1 iliyobainishwa katika Ripoti ya IMF WEO ya Oktoba 2025. Uchumi wa nchi ya Afrika Kusini unakadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 1.3 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 1.1 iliyobainishwa kwenye Ripoti ya Oktoba 2025. Aidha, Ripoti ya Januari 2026 inaendelea kubainisha kuwa kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi ya Nigeria kinakadiriwa kuwa asilimia 4.2 mwaka 2025 ikilinganishwa na makadirio ya ukuaji wa asilimia 4.1 yaliyobainishwa kwenye Ripoti ya Oktoba 2025.

1.3. Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Tathmini ya ukuaji wa uchumi kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka 2025 inaonesha kuwa, ukuaji wa uchumi wa Nchi ya Afrika Kusini uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 0.4 ambacho ni sawa na kiwango cha ukuaji katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Uchumi wa Nchi ya Namibia ulikua kwa kiwango hasi cha asilimia 0.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.2 kipindi

kama hicho mwaka 2024. Ukuaji wa uchumi wa Nchi ya Botswana ulikua kwa kiwango hasi cha asilimia 5.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa kiwango hasi cha asilimia 1.9 kipindi kama hicho mwaka 2024. Uchumi wa Tanzania uliongezeka hadi kiwango cha asilimia 5.7 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 5.4 kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha taarifa za mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025 bado hazijasambazwa kwenye tovuti za Ofisi za Takwimu za nchi husika.

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Robo ya Nne ya Mwaka 2024 na 2025




Chanzo: Tovuti za Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2025

1.4. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi za Jumuiya ya Afrika mashariki ambazo zimetoa taarifa za mwenendo wa shughuli za uchumi katika kipindi cha robo mwaka ya nne mwaka 2025 zilizopatikana kwenye tovuti za taasisi hizo zimeonesha kuendelea kuimarika kwa ukuaji chanya wa uchumi. Uchumi wa nchi ya Rwanda kwa robo mwaka ya nne 2025 umekua kwa kiwango cha asilimia 11.2 ukilinganisha na kiwango cha asilimia 4.2 kipindi kama hicho mwaka 2024. Uchumi wa nchi ya Uganda kwa robo mwaka ya nne ya mwaka 2025 umekua hadi kiwango cha asilimia 8.5 ukilinganisha na kiwango cha asilimia 5.4 kipindi kama hicho mwaka 2024. Kwa upande wa Tanzania uchumi umekua kwa kiwango cha asilimia 5.7 katika robo ya nne ya mwaka 2025 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.4 kipindi kama hicho mwaka 2024. Taarifa za mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika

Mashariki katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025 bado hazijasambazwa kwenye tovuti za Ofisi za Takwimu za nchi husika.

Kielelezo Na 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Nne Mwaka 2021 – 2025.



Chanzo: Tovuti za Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2025

1.5. Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa Nchini Tanzania

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaendelea kutekeleza sera ya mapitio ya takwimu za Pato la Taifa iliyoanza kutumika mwaka 2019. Sera hii inaruhusu kuchapisha matokeo ambayo yanaweza kufanyiwa mapitio kutokana na kupatikana kwa takwimu mpya au zilizofanyiwa mapitio za kila robo mwaka na kila mwaka. Kutokana na mapitio ya Sera hii na maboresho yaliyofanyika kwenye takwimu za urari wa biashara zinazotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, takwimu za Pato la Taifa zimefanyiwa mapitio kuanzia mwaka 2017 hadi 2024.

Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa katika kipindi cha robo ya nne (Oktoba hadi Desemba) 2025 umetumia taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli zote za kiuchumi zilizofanyika nchini.

1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Nne ya Mwaka 2025


Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025, Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika (*current prices*) liliongezeka hadi shilingi trilioni 62.5 kutoka shilingi trilioni 56.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, Pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka 2015 liliongezeka hadi Shilingi trilioni 44.4 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 kutoka Shilingi trilioni

42.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (**Jedwali Na 1**), ikiwa ni sawa na ongezeko halisi la asilimia 5.7 (**Kielelezo Na 3**).

Jedwali Na. 1: Thamani ya Pato la Taifa (TZS Milioni), Robo ya Nne Mwaka 2021-2025

Mwaka	Bei za Mwaka Husika	Bei za Mwaka 2015
2021	42,117,295	36,699,154
2022	46,253,804	37,956,359
2023	49,893,259	39,891,558
2024	56,433,470	42,049,933
2025	62,476,735	44,443,887

Kielelezo Na. 3: Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Nne ya Mwaka 2021 - 2025




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2025

1.5.2 Mchango wa Makundi Makuu ya Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa

Mchanganuo wa mchango wa makundi makuu ya shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 unaonesha kuwa, **Shughuli za Msingi** zilikuwa na mchango mkubwa zaidi wa **asilimia 43.3**, zikifuatiwa na **Shughuli za Huduma kwa asilimia 36.8** na **Shughuli za Kati** kwa **asilimia 19.9**. Mchango wa makundi makuu ya shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa umekokotolewa kwa bei za mwaka husika kabla ya kujumuisha kodi.

Kielelezo Na. 4: Mchango wa Makundi Makuu ya Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Robo ya Nne 2025




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2025

1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi, Robo ya Nne ya Mwaka 2025

Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025, Pato Halisi la Taifa (*constant 2015 prices*) liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.7 ikilinganishwa na asilimia 5.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Shughuli za kiuchumi zilizoongezeka kwa kasi kubwa zilikuwa ni Fedha na Bima (asilimia 19.5); Habari na Mawasiliano (asilimia 12.6); Umeme (asilimia 12.2); Afya na Huduma za Jamii (asilimia 12.0); Utawala na Ulinzi (asilimia 7.5); na Uchimbaji wa Madini na Mawe (asilimia 7.5); (Tazama Kielelezo Na.5).

Kielelezo Na.5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi, Robo ya Nne ya Mwaka 2025



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2025

1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Nne ya Mwaka 2025

Shughuli zote za uchumi zilizofanyika katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025 zilichangia katika ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.7 kwa viwango tofauti. Katika kipindi hicho, shughuli ya Kilimo ilikuwa na mchango mkubwa zaidi katika ukuaji kwa asilimia 20.5 ikifuatiwa na Fedha na Bima (asilimia 13.8); Ujenzi (asilimia 11.2); Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo (asilimia 8.4); Biashara na Matengenezo (asilimia 7.6); na Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 7.2).

2.0. Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi

Sura hii inabainisha kwa muhtasari shughuli za kiuchumi zilizofanyika pamoja na viwango vya ongezeko la thamani la shughuli hizo kati ya robo ya nne ya mwaka 2025 na robo ya nne ya mwaka 2024. Shughuli zilizobainishwa katika sura ndogo za sura ya pili ni kilimo cha mazao, ufugaji, misitu na uvuvi. Shughuli nyingine ni uchimbaji madini na mawe; uzalishaji viwandani, umeme, maji na ujenzi. Aidha, shughuli nyingine ni biashara na matengenezo; usafirishaji na uhifadhi wa mizigo; malazi na huduma za chakula; habari na mawasiliano; fedha na bima; upangishaji majengo, huduma za kitaalam, ufundi na sayansi; huduma

zinazohusiana na utawala, utawala na ulinzi, elimu, afya na huduma za jamii, sanaa na burudani; na huduma nyingine za jamii.

2.1. Kilimo, Misitu na Uvuvi


Shughuli hizi zinahusika na uvunaji wa rasilimali za asili za mazao, wanyama na samaki. Shughuli hizi zinajumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili na uvuvi. Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2025, shughuli ya kilimo iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 4.4 ikilinganishwa na asilimia 4.2 kipindi kama hicho mwaka 2024.

2.1.1. Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa katika shughuli ya kilimo cha mazao ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyingine, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharage, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli ndogo ya mazao iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.3 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao uliotokana na matumizi ya teknolojia na pembejeo bora pamoja na kuendelea kuimarika kwa huduma za ugani.

Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Nne ya Mwaka 2024 na 2025



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2025

Mazao ya kilimo yaliyochangia zaidi katika ukuaji wa shughuli ya mazao katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ni pamoja na: mahindi, mpunga, maharage na kunde; na korosho. Katika kipindi hicho, uzaishaji wa mahindi uliongezeka kwa asilimia 7.0 kutoka tani milioni 4.3 mwaka 2024 hadi tani milioni 4.6 mwaka 2025, uzalishaji wa mpunga uliongezeka

kwa asilimia 9.3 kutoka tani elfu 952 mwaka 2024 hadi tani milioni 1.0 mwaka 2025. Aidha, maharage na mikunde iliongezeka kwa asilimia 3.3 kutoka tani elfu 455 mwaka 2024 hadi tani elfu 470 mwaka 2025. Vilevile, korosho iliongezeka kwa asilimia 0.9 kutoka tani elfu 107 hadi tani elfu 108 mwaka 2025.

2.1.2. Mifugo

Shughuli hii inahusika na ufugaji ng'ombe wa asili na wa kisasa; mbuzi, kondoo, punda, farasi, nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyingine.

Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka 2025, ongezeko la thamani linalotokana na mifugo liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.0 ambacho ni sawa na kiwango cha ukuaji katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za mifugo na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa kutumia lishe bora inayotokana na mazao ya Mifugo.

2.1.3. Misitu

Shughuli hii inahusu uzalishaji wa mbaao, mkaa, kuni na magogo, matawi, fungu la matawi na mazao ya misitu yasiyo ya kuni. Shughuli hii iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 3.3 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 2.9 kipindi kama hicho mwaka 2024. Kasi ya ukuaji huu ilitokana na kuongezeka kwa usimamizi wa rasilimali za misitu pamoja na juhudi za Serikali katika kuhakikisha uvunaji endelevu wa bidhaa za misitu.

2.1.4. Uvuvi

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi. Shughuli za uvuvi ziliongezeka hadi kiwango cha asilimia 3.1 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 2.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kasi ya ukuaji wa shughuli ya uvuvi ilitokana na juhudi za Serikali katika kusimamia uvunaji wa mazao ya uvuvi.

2.2. Uchimbaji wa Madini na Mawe

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe inahusisha uchimbaji au ukusanyaji wa madini yabisi yanayopatikana kwenye uso wa dunia kama vile makaa ya mawe na chuma; vimiminika (mfano petroli) au gesi (mfano gesi asilia). Uchimbaji wa madini na mawe hufanyika chini ya ardhi, ukusanyaji kutoka juu ya ardhi au kwenye visima. Uchimbaji wa madini na mawe pia unajumuisha shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha. Shughuli hizi mara nyingi zinatekelezwa na vitengo rasmi ambavyo vinavuna rasilimali za madini na vingine vilivyopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe imegawanyika katika maeneo makuu manne ambayo ni:

- i. Madini ya makaa ya mawe;
- ii. Petroli na gesi asilia;
- iii. Uchimbaji wa madini ya chuma; na
- iv. Madini ya kokoto na mawe.

Shughuli ya uchimbaji madini na mawe iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 7.5 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 8.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mabadiliko katika kasi ya ukuaji yalitokana na ongezeko la uzalishaji kwenye baadhi ya madini ikiwemo Dhahabu, madini ya Fedha, Phosphate, Mawe ya chokaa, pozzolana na madini ya chuma. (Tazama **Jedwali Na.1**).

Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Baadhi ya Madini kwa Robo ya Nne ya Mwaka 2024 na 2025

Aina ya Madini	Kipimo	Robo ya Nne	
		2024	2025
Dhahabu	Kg	17,637	17,685
Fedha	Kg	226	973
Phosphate	Tani	6,602	16,350
Mawe ya Chokaa	Tani	2,914,803	3,322,380
Pozzolana	Tani	112,636	213,184
Chuma	Tani	12,253	33,060

Chanzo: Wizara ya Madini, 2025

2.3. Uzalishaji Viwandani

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa kutoka katika hali yake ya kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa za viwandani zinazochakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi na madini.

Shughuli ya uzalishaji viwandani iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 4.2 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 3.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huu ulichangiwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

2.4. Umeme

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme ni kutoka katika vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Shughuli hii inahusika na usambazaji na ugawaji wa umeme. Vyanzo vikuu vya takwimu za uzalishaji wa umeme ni kutoka katika kampuni za uzalishaji wa umeme za TANESCO.

Ukuaji wa shughuli ya uzalishaji wa nishati ya umeme hutegemea kiasi cha umeme kilichozalishwa na kusambazwa kwa wateja mbalimbali. Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025, shughuli ya uzalishaji umeme iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 12.2 kutoka asilimia 23.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huu ulichangiwa na uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo ya kuzalisha umeme kutumia jua (Solawazi), umeme ulionunuliwa kutoka Kenya na kuendelea kuzalishwa kwa umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere.


2.5. Usambazaji Maji

Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Vilevile, shughuli hii inahusika na ukusanyaji wa maji taka.

Kiashiria cha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji ni kiasi cha maji kilichozalishwa. Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025, kiasi cha maji kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 107.1 kutoka mita za ujazo milioni 104.5 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Tazama **Kielelezo 7**).

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji kiliongezeka kwa asilimia 2.5 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 kutoka asilimia 5.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2024.

Kielelezo Na. 7: Uzalishaji wa Maji, Robo ya Nne Mwaka 2021 – 2025



Chanzo: Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, 2025

2.6. Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa aina zote na shughuli maalum za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii inajumuisha pia ujenzi mpya, ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo na ujenzi wa miundombinu.

Shughuli za ujenzi zinajumuisha, ujenzi wa nyumba za kuishi na nyumba za makazi, ujenzi wa majengo ya biashara au ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Shughuli hii pia inajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya majitaka, miundombinu ya viwanda, mabomba, mifumo ya umeme na vituo vya michezo.

Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025, shughuli ya ujenzi ilikuwa hadi kiwango cha asilimia 4.9 ikilinganishwa na asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Tathmini ya ukuaji wa shughuli ya ujenzi hutumia viashiria vya uzalishaji wa bidhaa za ndani pamoja na zilizoagizwa kutoka nchi za nje zinazotumika katika ujenzi. Bidhaa za ndani zilizochangia ukuaji wa shughuli hii katika kipindi husika ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa saruji na bidhaa za chuma.

2.7. Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inajumuisha uuzaji wa jumla na rejareja (uuzaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko ya bidhaa) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa. Pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji wa mitambo na ukarabati wa bidhaa binafsi za nyumbani. Shughuli kuu inayohusisha biashara na matengenezo ni kununua na kuuza bidhaa.

Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025, ukuaji wa shughuli ya biashara na matengenezo iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.1 ikilinganishwa na asilimia 5.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa ikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, mifugo, uvuvi, madini, bidhaa za viwandani na zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

2.8. Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo

Shughuli hii inajumuisha huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, iliyoratibiwa au bila kuratibiwa, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana kama vile kushughulikia mizigo, kuhifadhi n.k. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri vikiwa na dereva au mwendesha mitambo na shughuli za posta na barua. Shughuli hii iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 6.8 katika robo ya nne ya mwaka 2025 kutoka asilimia 1.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na ongezeko la mizigo na idadi ya abiria waliosafirishwa kwa huduma za usafiri wa barabarani na pia treni ya mwendo kasi.

2.9. Malazi na Huduma ya Chakula

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa malazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine. Pia huduma tajwa inahusisha utoaji wa milo na vinywaji kamili kwa matumizi ya haraka. Kiasi na aina ya huduma za ziada zinazotolewa ndani ya sehemu hii zinaweza kutofautiana sana.

Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025, kiwango cha ukuaji wa huduma za malazi na chakula ziliongezeka kwa asilimia 1.5 ikilinganishwa na asilimia 5.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulichangiwa na kupungua kwa idadi ya watalii walioingia nchini. Katika kipindi cha Oktoba Disemba 2025, Idadi ya watalii walioingia nchini ilipungua kutoka watu 581,254 mwaka 2024 hadi 562,971, ikiwa ni kiwango hasi cha asilimia 3.1.

2.10. Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji kama vile utangazaji wa redio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari ikiwa ni pamoja na uchakataji wa taarifa.


Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya habari na mawasiliano kilikuwa asilimia 12.6 katika robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 15.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na kuongezeka kwa muda wa kuongea kwa simu, huduma ya utumaji ujumbe mfupi na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu pamoja na huduma za utangazaji na huduma za intaneti kwa ujumla.

2.11. Fedha na Bima

Shughuli hizi zinahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Huduma ya fedha na bima iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 19.5 katika robo ya nne ya mwaka 2025 kutoka asilimia 12.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na kuongezeka kwa asilimia 25.7 kwa amana za wateja kutoka shilingi trilioni 40.1 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2024 hadi shilingi trilioni 50.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Vile vile, kuongezeka kwa asilimia 23.9 kwa mikopo kutoka shilingi trilioni 37.3 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2024 hadi shilingi trilioni 46.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2025.

Kielelezo Na. 8: Thamani ya Mikopo na Amana (TZS Trilioni), Robo ya Nne ya Mwaka 2021 – 2025



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2025

2.12. Upangishaji Majengo

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, majengo na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoja na kupima mali isiyohamishika kama vile viwanja.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya upangishaji majengo kilifikia asilimia 4.4 katika robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko la mahitaji ya huduma za malazi hususan katika maeneo ya mjini lilichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

2.13. Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalum za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa

huduma kwa watumiaji. Shughuli hii inahusisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalum wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Kasi ya ukuaji wa shughuli hii ilikuwa asilimia 5.3 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 5.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa shughuli za kitaalam, ufundi na sayansi katika kipindi husika.

2.14. Huduma zinazohusiana na Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia kufanyika kwa biashara ambazo ni pamoja na huduma za kukodisha vifaa, ajira, uwakala wa kampuni za usafiri, kuongoza watalii, kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli hii kilikuwa asilimia 3.4 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 8.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kuongezeka kwa huduma za uwakala wa usafiri wa watalii ulichangia ukuaji wa shughuli hii ya kiuchumi.

2.15. Utawala na Ulinzi

Shughuli za Utawala na Ulinzi zinahusika na kutunga na kutafsiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi wa mipaka ya nchi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla. Aidha, huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima imejumuishwa katika shughuli ya Utawala na Ulinzi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya utawala na ulinzi ilikuwa asilimia 7.5 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilima 8.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya fedha za Serikali katika kulipa mishahara, kulipa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi na wazabuni na utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla.

2.16. Elimu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu kwa njia ya kuongea au maandishi, kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano katika ngazi zote za sekta ya Elimu. Vilevile, inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi mbalimbali katika mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu katika sekta ya umma na binafsi.

Shughuli ya elimu iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.0 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 kutoka asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji wa shughuli hii ulitokana na udahili wa wanafunzi katika ngazi zote za utoaji wa elimu za umma na binafsi.

2.17. Afya na Huduma za Jamii

Huduma za Afya na Jamii zinajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii zinazotolewa na wataalam wa matibabu katika hospitali na vituo vingine. Pia inahusisha shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalam wa huduma za afya.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya utoaji wa huduma za afya kilifikia asilimia 12.0 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 11.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote za kutolea huduma.

2.18. Sanaa na Burudani

Shughuli hii inajumuisha shughuli mbalimbali za kitamaduni na burudani kwa manufaa ya umma kwa ujumla ikiwa ni pamoja na sanaa ya maonesho, uendeshaji wa makumbusho, kamari, michezo na shughuli za burudani.

Kasi ya ukuaji wa shughuli hii ilikuwa asilimia 5.8 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 15.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kiwango cha ukuaji wa shughuli hii kilitokana na kuendelea kuongezeka kwa shughuli za sanaa na burudani .

2.19. Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijumuishwi kwenye shughuli nyingine. Pia inajumuisha shughuli ya sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri.

Kasi ya ukuaji wa shughuli hii ilifikia asilimia 6.2 katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kiwango cha ukuaji wa shughuli hii kilitokana na kuendelea kuongezeka kwa utoaji wa huduma katika maeneo ya mjini na mahitaji ya huduma za jamii kwa ujumla.

3.0. Hitimisho

Katika robo ya nne ya mwaka 2025, Pato halisi la Taifa liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.7 ikilinganishwa na asilimia 5.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Shughuli za kiuchumi zilizoongezeka kwa kiwango kikubwa zilikuwa pamoja na: Fedha na Bima (asilimia 19.5); Habari na Mawasiliano (asilimia 12.6); Umeme (asilimia 12.2); Afya na Huduma za Jamii (asilimia 12.0); Utawala na Ulinzi (asilimia 7.5); na Uchimbaji wa Madini na Mawe (asilimia 7.5).

Viambatanisho:

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 - Sh. Milioni

Mwaka	Robo	Kilimo	Uchimbaji Madini na Mawe	Viwandani	Umeme	Maji Safi na Maji Taka	Ujenzi	Biashara na Matengenezo	Malazi na Huduma za chakula	Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima
2012		21,807,030	3,314,742	6,066,989	669,069	358,361	7,578,263	7,371,411	1,343,924	5,710,466	1,266,747	3,444,161
2013		22,408,192	3,464,721	6,292,514	723,608	367,890	9,023,353	7,682,286	1,356,204	6,050,976	1,414,116	3,405,940
2014		23,952,077	3,687,273	6,919,794	815,297	381,760	9,253,082	8,444,243	1,397,782	6,577,706	1,560,064	3,764,113
2015		25,234,560	4,055,619	7,411,672	798,801	390,758	10,446,797	8,747,862	1,421,916	6,929,895	1,681,098	4,189,021
2016		26,436,338	4,356,709	8,213,364	869,262	417,899	11,960,720	9,260,703	1,480,052	7,324,856	1,718,548	4,235,515
2017		27,999,284	4,588,624	8,889,818	877,667	444,660	13,765,005	9,829,967	1,525,619	7,815,845	1,824,472	4,115,393
2018		29,504,236	4,659,195	9,623,501	928,174	477,510	15,655,747	10,480,204	1,604,391	8,736,561	1,989,717	4,094,972
2019		30,802,622	5,485,112	10,184,558	994,879	510,411	17,737,886	10,984,480	1,645,950	9,493,191	2,133,312	4,281,167
2020		32,323,673	5,887,452	10,646,279	1,049,610	540,159	19,128,358	11,216,401	1,419,654	10,293,276	2,313,032	4,412,967
2021		33,588,777	6,442,881	11,155,762	1,154,204	575,213	19,757,591	11,578,146	1,514,711	10,658,344	2,524,610	4,599,677
2022		34,711,277	7,138,149	11,624,144	1,242,132	606,754	20,536,757	12,031,598	1,651,099	11,061,950	2,712,411	5,024,301
2023		36,184,322	7,945,921	12,128,562	1,290,960	621,827	21,247,110	12,542,371	1,788,242	11,510,657	2,917,297	5,760,339
2024		37,677,355	8,605,295	12,712,638	1,477,093	647,165	22,123,264	13,142,577	1,895,759	11,990,434	3,334,136	6,557,881
2012	1	5,972,854	845,470	1,528,195	151,473	86,422	1,816,993	1,877,418	321,003	1,208,445	281,981	849,590
	2	5,182,996	825,383	1,544,666	164,427	89,319	1,808,760	1,855,404	320,427	1,456,176	303,507	844,631
	3	4,092,001	833,592	1,499,895	172,946	92,526	2,012,312	1,725,714	358,248	1,489,645	327,526	886,247
	4	6,559,178	810,297	1,494,233	180,223	90,094	1,940,197	1,912,875	344,245	1,556,199	353,733	863,692
2013	1	5,994,220	748,412	1,459,422	167,460	87,306	2,146,785	1,828,162	332,454	1,519,508	312,238	811,387
	2	5,376,452	850,463	1,547,040	177,004	90,069	2,111,891	1,884,307	324,659	1,501,581	343,060	836,571
	3	4,199,755	875,290	1,677,731	181,477	85,918	2,389,873	1,893,295	354,104	1,513,039	358,452	881,698
	4	6,837,765	990,556	1,608,322	197,667	104,598	2,374,804	2,076,522	344,987	1,516,849	400,366	876,284
2014	1	6,335,448	937,448	1,621,405	201,849	87,893	2,182,230	2,054,479	346,623	1,625,429	342,909	912,095
	2	5,877,120	871,899	1,706,772	182,845	94,708	2,507,336	2,073,942	339,327	1,616,710	380,305	927,895
	3	4,450,294	929,381	1,788,128	213,998	97,099	2,228,708	2,035,245	361,470	1,686,150	414,058	960,721
	4	7,289,215	948,546	1,803,489	216,605	102,059	2,334,808	2,280,578	350,362	1,649,417	422,793	963,401
2015	1	6,605,887	923,326	1,733,636	211,828	96,862	2,438,046	2,093,973	346,778	1,654,599	386,446	995,846
	2	6,347,239	965,335	1,820,111	199,281	92,862	2,690,105	2,195,254	345,054	1,676,064	412,841	1,011,653
	3	4,656,388	960,427	1,939,664	192,215	99,585	2,601,253	2,162,776	372,080	1,764,202	441,478	1,076,143
	4	7,625,045	1,206,532	1,918,260	195,477	101,448	2,717,393	2,295,860	358,003	1,835,030	440,334	1,105,380
2016	1	6,788,342	1,017,609	1,965,656	214,850	95,779	2,859,933	2,295,506	358,142	1,818,390	401,047	1,111,056
	2	6,853,095	1,109,064	1,996,019	210,034	100,816	2,995,869	2,318,553	347,167	1,819,827	421,552	1,052,954
	3	4,936,684	1,098,979	2,080,908	214,673	103,584	3,208,669	2,300,383	385,323	1,854,653	451,160	1,053,955
	4	7,858,218	1,131,055	2,170,783	229,706	117,720	2,896,249	2,346,262	389,420	1,831,986	444,789	1,017,550
2017	1	7,232,687	1,118,373	2,067,899	223,826	97,295	3,204,078	2,340,748	374,854	1,914,669	451,535	1,046,336
	2	7,283,393	1,057,691	2,187,504	207,471	105,045	3,631,267	2,439,389	359,355	1,910,951	448,743	1,028,316
	3	5,137,220	1,144,597	2,365,766	222,983	113,969	3,198,026	2,436,482	395,146	1,982,315	459,599	998,080

Muhtasari wa Pato la Taifa - Robo ya Nne

Mwaka	Robo	Kilimo	Uchimbaji Madini na Mawe	Viwandani	Umeme	Maji Safi na Maji Taka	Ujenzi	Biashara na Matengenezo	Malazi na Huduma za chakula	Usafirishaji na Uhifadhi Mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima
	4	8,345,985	1,267,964	2,268,650	223,386	128,352	3,731,635	2,613,347	396,263	2,007,909	464,595	1,042,661
2018	1	7,717,887	1,054,655	2,173,169	225,315	100,913	3,703,467	2,452,093	391,664	2,082,426	522,189	1,017,429
	2	7,716,454	1,129,287	2,259,893	221,260	111,470	3,846,566	2,543,415	383,333	2,169,733	506,979	1,004,585
	3	5,333,853	1,166,716	2,530,756	235,524	126,137	3,711,275	2,626,676	425,407	2,222,813	481,221	1,036,203
	4	8,736,041	1,308,537	2,659,683	246,075	138,991	4,394,440	2,858,020	403,987	2,261,589	479,328	1,036,756
2019	1	8,180,843	1,159,804	2,280,570	248,981	108,984	4,201,084	2,536,964	390,255	2,312,794	563,425	1,068,986
	2	8,024,755	1,323,857	2,384,031	239,830	118,551	4,636,133	2,678,200	393,345	2,322,004	538,389	1,046,643
	3	5,519,940	1,413,025	2,749,036	247,877	139,826	4,314,813	2,795,019	442,538	2,407,844	516,803	1,085,094
	4	9,077,084	1,588,425	2,770,921	258,191	143,049	4,585,856	2,974,297	419,812	2,450,548	514,695	1,080,444
2020	1	8,499,072	1,365,988	2,387,165	264,556	116,821	4,412,066	2,659,968	400,323	2,505,607	609,865	1,116,244
	2	8,358,112	1,438,625	2,479,030	247,959	124,044	5,138,451	2,672,450	330,902	2,541,456	592,089	1,079,729
	3	5,861,379	1,491,966	2,886,991	258,775	150,811	4,897,568	2,866,000	331,271	2,576,818	561,022	1,105,717
	4	9,605,109	1,590,872	2,893,092	278,320	148,483	4,680,272	3,017,983	357,157	2,669,394	550,056	1,111,277
2021	1	8,676,345	1,489,458	2,532,535	283,025	127,311	4,604,173	2,720,432	374,418	2,730,301	663,760	1,136,964
	2	8,565,701	1,574,503	2,589,415	277,449	134,491	5,165,141	2,783,693	364,386	2,666,798	661,706	1,113,879
	3	6,148,484	1,677,259	2,995,394	284,709	157,663	5,121,115	2,909,425	378,526	2,560,195	607,185	1,150,583
	4	10,198,247	1,701,661	3,038,419	309,022	155,747	4,867,162	3,164,596	397,381	2,701,050	591,959	1,198,251
2022	1	9,041,413	1,634,049	2,692,630	309,554	142,426	4,901,874	2,915,160	379,909	2,765,442	703,102	1,246,351
	2	8,891,172	1,665,101	2,711,874	304,216	147,326	5,316,913	2,969,053	411,599	2,775,195	704,239	1,221,978
	3	6,387,399	1,838,926	3,127,447	312,261	157,751	5,215,685	2,964,425	428,373	2,746,367	672,848	1,250,951
	4	10,391,293	2,000,074	3,092,193	316,101	159,251	5,102,285	3,182,960	431,217	2,774,947	632,221	1,305,020
2023	1	9,489,715	1,865,822	2,836,543	320,758	149,709	5,151,185	2,993,190	426,514	2,829,232	727,646	1,399,683
	2	9,164,423	1,840,260	2,828,374	322,973	152,131	5,437,956	3,090,258	441,387	2,884,703	747,707	1,392,927
	3	6,716,865	2,102,597	3,258,720	322,508	160,561	5,407,274	3,092,198	460,161	2,893,049	748,551	1,460,968
	4	10,813,320	2,137,242	3,204,925	324,721	159,426	5,250,696	3,366,725	460,180	2,903,672	693,393	1,506,762
2024	1	9,724,951	1,930,403	3,000,466	345,257	154,294	5,481,115	3,150,509	457,039	2,990,585	834,062	1,607,738
	2	9,641,700	1,962,805	2,959,633	358,409	157,507	5,597,773	3,204,215	465,811	2,988,433	844,477	1,589,059
	3	7,045,833	2,394,128	3,421,790	370,987	166,494	5,618,247	3,240,435	486,709	3,059,351	857,347	1,672,481
	4	11,264,869	2,317,959	3,330,748	402,440	168,870	5,426,128	3,547,418	486,200	2,952,064	798,249	1,688,602
2025	1	10,018,797	2,250,262	3,215,745	410,806	160,747	5,716,166	3,260,943	467,535	3,184,291	898,989	1,855,362
	2	10,037,062	2,335,835	3,103,792	408,667	163,408	5,889,135	3,381,546	484,036	3,118,796	938,143	1,823,453
	3	7,403,238	2,564,637	3,577,271	421,401	173,751	5,980,844	3,447,956	519,089	3,253,368	963,218	1,910,433
	4	11,756,650	2,491,365	3,471,208	451,421	173,015	5,694,556	3,728,197	493,501	3,154,018	898,608	2,017,856

Kiambatisho Na. 1 (Kinaendelea.): Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni

Mwaka	Robo	Utawala na ulinzi	Shughuli za Kitaaluma, Sayansi na Ufundi	Huduma zinazohusiana na Utawala	Upangishaji Majengo	Elimu	Afya na Huduma za Jamii	Sanaa na Burudani	Huduma nyingine za Kijamii	Jumla ya Ongezeko la Thamani	Ongeza kodi katika bidhaa	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko
2012		3,623,123	322,260	1,417,467	2,606,439	1,922,643	1,284,594	230,652	711,918	71,050,258	6,961,771	78,012,029
2013		3,974,206	385,090	1,660,994	2,714,775	1,927,633	1,245,030	212,502	778,959	75,088,988	8,179,129	83,268,117
2014		4,242,164	447,921	1,976,260	2,828,970	2,186,260	1,349,941	230,652	857,665	80,873,021	8,001,090	88,874,111
2015		4,548,604	518,123	2,183,917	2,949,598	2,413,306	1,419,090	248,510	895,589	86,484,736	7,864,579	94,349,316
2016		4,793,820	606,207	2,611,498	3,077,086	2,665,336	1,497,896	280,131	997,915	92,803,857	8,024,535	100,828,393
2017		4,907,113	694,291	2,892,463	3,211,895	2,859,171	1,611,999	307,907	1,101,598	99,262,789	8,348,602	107,611,391
